

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA SIKU YA KUPIGA KURA.**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani utafanyika siku ya Jumapili tarehe 25/10/2015. Wananchi wote mnakumbushwa;

- Kufika katika Vituo vya Upigaji Kura katika muda uliotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambao ni Saa 1:00 Asubuhi hadi Saa 10:00 Jioni.
- Kutokuvaa sare zinazokutambulisha kuwa wewe ni mfuasi wa Chama Fulani cha Siasa.
- Kila Mpiga kura atapiga kura katika Kituo alichojiandikishia atatakiwa kuonyesha Kadi yake kama uthibitisho kuwa yeye ni Mpiga kura.
- Msimamizi wa Kituo atahakiki jina la Mpiga Kura huyo kama lipo katika Daftari la Kituo hicho.
- Ikumbukwe pia kuwa watu wenye Mahitaji Maalumu kama watu Wenye Ulemavu wa aina yoyote ile, Wanawake Wajazito na Wazee watapewa kipaumbele.
- Kwa Vyama vya Siasa Tume inawaasa kuzingatia Sheria na Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015 kama yalivyochapishwa kwenye TANGAZO LA SERIKALI NA 294 la tarehe 27 JULAI 2015, ambapo Vyama vya Siasa vitakatikwa kuzingatia mambo yafuatayo;
  1. Kuheshimu na kutekeleza Sheria za Uchaguzi, Kanuni za Uchaguzi, Maadili ya Uchaguzi na **Maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi** pamoja na Sheria zingine za Nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi
  2. Viongozi wa Vyama vya Siasa na Wagombea **wawaelimishe Wanachama** wao kutekeleza Sheria za Uchaguzi, Sheria zingine za Nchi, Kanuni na Taratibu zilizopo.
  3. Vyama vyote vya Siasa, Wagombea, Wanachama na Wafuasi wa Vyama vya Siasa wahakikishe kwamba wanafanya hatua za makusudi; Kufanya Uchaguzi ulio huru na haki, Kukataa na kulaani vitendo vya vurugu na vitisho, Kueneza taarifa sahihi kuhusiana na mchakato wa Uchaguzi.

**Maadili ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 yaliyosainiwa na Vyama vyote vya Siasa tarehe 27 Julai, 2015 yatachapwa katika Magazeti mbalimbali Nchini kesho tarehe 23/10/2015.**

**KURA YAKO MUSTAKABALI WAKO, NENDA UKAPIGE KURA JUMAPILI TAREHE 25 OKTOBA, 2015  
KATIKA KITUO ULICHOJIANDIKISHIA UKIWA NA KADI YAKO.**

**Tangazo Hili Limetolewa na:**

**Tume ya Taifa ya Uchaguzi S. L. P 10932 Dar es Salaam**